

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI**



USAJILI WA WATAALAMU WA MABWAWA

Kwa Mujibu wa Kifungu cha 86 ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na.11 ya mwaka 2009 pamoja na Kanuni za Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Usalama wa Mabwawa) za mwaka 2013 zilizotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 237, Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji anawatangazia wataalamu wote wanaofanya kazi zinazohusiana na mabwawa ambazo ni pamoja na usanifu, ujenzi, ukarabati, uboreshaji, uendeshaji, ufuatiliaji, ukaguzi, uzinduzi au ufungaji wa mabwawa ya maji na/au mabwawa ya kuhifadhi mabaki ya taka za migodini (topesumu) kwamba wanatakiwa kusajiliwa na Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kama wataalamu walioidhinishwa (Approved Professional Persons). Ili kusajiliwa, mtaalamu anatakiwa awe na sifa zifuatazo:

- a) Shahada ya Sayansi katika fani za Uhandisi Ujenzi, Mitambo, Umeme, *Hydraulics*, Mazingira na Rasilimali za Maji au fani zinazofanana na hizo;
- b) Uzoefu usiopungua miaka mitano kwenye shughuli za mabwawa ambazo ni pamoja na usanifu, ujenzi, ukarabati, uboreshaji, uendeshaji, ufuatiliaji, ukaguzi, uzinduzi au ufungaji wa mabwawa na/au mabwawa ya kuhifadhi mabaki ya taka za migodini (topesumu);
- c) Awe amesajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*).

Mwombaji ajaze fomu inayopatikana kwenye tovuti ya Wizara, ambapo maelezo ya ziada yanapatikana (www.maji.go.tz) kisha aiwasilishe kwa Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kwa anuani iliyoandikwa hapa chini. Fomu hiyo pia inaweza kupatikana katika ofisi ya Mkurugenzi.

Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji,
Wizara ya Maji,
NBC Tawi la Mazengo – Barabara ya Kuu,
S.L.P. 456,
40473, Dodoma. Barua pepe: dwr@maji.go.tz

Maombi yaambatane na wasifu wa mwombaji. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 28 Februari, 2019. Katazo linatolewa kwa mtalaamu yeyote kujishughulisha na kazi za mabwawa kuanzia tarehe 01/04/2019 bila kusajiliwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na. 11 ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2013, ni kosa kwa mtu yeyote kujishughulisha na kazi za usalama wa mabwawa pasipo kusajiliwa.

Dkt. George V. Lugomela
KAIMU MKURUGENZI WA RASILIMALI ZA MAJI
17 Disemba 2018